



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO
BODI YA FILAMU TANZANIA
TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**



**KUTAMBULISHA FILAMU ZILIZOPITA KWENYE MCHUJO WA AWALI WA TUZO ZA
FILAMU 2023**

Dar es Salaam - 31 Oktoba 2023

Katika kuunga mkono jitihada za Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za kuimarisha program zinazotambua, kutangaza na kuendeleza vipaji vya Wasanii wetu, Serikali kupitia Bodi ya Filamu Tanzania ilianzisha Programu ya Tuzo za Filamu mwaka 2021. Nia ya Serikali ya kuanzisha Programu hii ambayo Wadau wa Sekta ya Filamu Tanzania wanaofanya vizuri zaidi kwenye maeneo yao ya ubobevu hutunukiwa Tuzo na Serikali ni:

1. Kutambua mchango wao,
2. Kutambua vipaji vyao,
3. Kuwaongezea hamasa ya kuzalisha kazi nyingi zaidi za filamu,
4. Kuwaongezea hamasa ya kuzalisha kazi zenye ubora zaidi ili wawe na ushindani mkubwa ndani na nje ya nchi, na
5. Kuibua fursa za uwekezaji katika eneo hilo la Filamu nchini.

Serikali kupitia Bodi ya Filamu ilifungua rasmi dirisha la upokeaji wa Filamu kwa ajili ya Tuzo za Filamu Msimu wa Tatu wa Tamasha la Tuzo za Filamu Tanzania 2023 (Tanzania Film Festival Awards 2023 - TAFFA) tarehe 11 Agosti, 2023.

Kamati ya Sekretarieti ya Tuzo za Filamu inayoundwa na Maafisa Filamu kutoka Bodi ya Filamu, Watendaji, pamoja na wadau mbalimbali wa Filamu ilifika Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara kwa lengo la kupokea Filamu zitakazowania Tuzo. Aidha, Tamasha la Tuzo la Filamu 2023 limetanua wigo na kuanzisha Kipengele kipya cha Filamu za lugha ya Kiswahili kutoka Nchi za Afrika Mashariki.

Jumla ya Filamu 565 zilipokelewa kwa nia ya kushiriki katika vipengele vya Tuzo za mwaka 2023 ambapo Filamu 535 zimetoka Tanzania na Filamu 30 kutoka nje ya Tanzania katika Nchi za Kenya, Uganda na DRC. Baada ya zoezi la ukusanyaji wa Filamu hizo kukamilika, lilifuatiwa na zoezi la uchambuzi wa Filamu ambapo zilipatikana Filamu 204 kutoka kwenye Filamu za Tanzania na Filamu zote 30 za Kipengele cha Afrika Mashariki.

Filamu zilizoipita kwenye mchujo wa awali katika misimu miwili iliyopita ya Tamasha la Tuzo za Filamu zilioneshwa kwenye Kituo cha Televisheni cha Azam Media kupitia Chaneli ya Sinema Zetu, Na. 103. Filamu za msimu wa mwaka 2023 pia zitaoneshwa kupitia Kituo hicho na katika Vituo vingine vya Televisheni ambavyo Muandaaji wa kazi husika ataridhia kuoneshwa filamu yake.

Pamoja na mambo mengine, Tamasha la Tuzo za Filamu 2023 limeboreshwa katika maeneo sita (6) ya kiutendaji, hususan kwenye eneo la ubora wa Tamasha la Tuzo kama ifuatavyo:

1. Idadi ya Filamu zilizopita mchujo wa Awali ni kubwa zaidi kulinganisha na miaka ya nyuma. Mwaka Jana jumla ya Filamu 189 zilipita mchuo kati ya Filamu 840 zilizopokelewa. Lakini mwaka huu jumla ya filamu 204 zimefaulu katika hatua hii ya awali kati ya filamu 565 zilizopokelewa. Kitakwimu, mwaka huu 41% ya Filamu zilizopokelewa zimefaulu, ikiwa ni ongezeko la 18% kutoka 23% ya Filamu zilizofaulu mwaka Jana.
2. Eneo la Ukuaji: mwaka 2023, Tuzo zimefungua milango ya Filamu za Kimataifa (Afrika Mashariki) ambapo kutakuwa na vipengele vya:
 - a. Filamu Ndefu Bora za Kiswahili
 - b. Tamthilia Bora za Kiswahili
3. Uoneshaji wa Filamu utakuwa huru kwa Kituo chochote kitakachoweza kuonesha Filamu hizo badala ya Azam pekee kama ilivyokuwa kwa miaka iliyopita 2021 na 2022
4. Utatumika muda mrefu zaidi kwenye zoezi la kufanya *Judgement*. Utaratibu huu utasaidia kuongeza ufanisi wa kupata Filamu bora na Washindi sahihi.
5. Tumeongeza njia ya kupokea Filamu kwa MTANDAO, ambapo miaka ya nyuma tulipokea Filamu kwa njia ya kuwasilishwa ofisini na kuzifuata mikoani pekee. Aidha mwaka huu, tumefika mikoa yote ya Tanzania Bara badala ya mikoa 25 kwa mwaka jana na mikoa 7 pekee kwa mwaka Juzi.
6. Majaji wataamua vipengele vya kushindaniwa katika kila Filamu. Miaka ya nyuma, Wazalishaji walikuwa wanaamua wao na wakati mwingine kusababisha Wasanii wao kutoshinda vipengele hivyo kutokana na kukosea kuchagua vipengele ambavyo Wasanii hao wamefanya vizuri zaidi. Hatua hii imekuja baada ya kuangalia Nchi nyingine zinavyofanya kwenye Tuzo zao. Tunaamini hatua hii itapunguza sana malalamiko ya Wasanii waliokuwa wanahisi kutotendewa haki katika ushindani.

Sambamba na hayo, Bodi ya Filamu Tanzania inaendelea kutoa rai kwa wadau na mashabiki wa Filamu kuendelea kufuatilia muendelezo wa Tamasha la Tuzo za Filamu 2023, kupitia Tovuti ya www.filmboard.go.tz pamoja na mitandao ya Kijamii Instagram @tanzania_film_board, Twitter @Bodi_FilamuTz, Facebook @Bodi Ya Filamu Tanzania na YouTube @bodi ya Filamu Online Tv.

Imetolewa na BODI YA FILAMU TANZANIA